Neno hili linatwa mara nyingi sana katika biblia, sana sana mahali ambavyo vinatajwa vizazi vya wana wa Israeli.

Mbari, kwa jina lingine ni UKOO. Kwamfano unaweza kukutana na sehemu fulani inasema, “hawa ndio wakuu wa mbari za baba zao”. Hapo inamaanisha kuwa “hao ndio wakuu wa ukoo wa baba zao”,

Vifuatavyo ni baadhi ya vifungu ambavyo utakutana na Neno hilo;

> *1Wafalme 8:1 “Ndipo Sulemani alipowakusanya wazee wa Israeli, na wakuu wote wa kabila, wakuu wa mbari za mababa wa wana wa Israeli, wamwendee mfalme Sulemani huko Yerusalemu, ili walipandishe sanduku la agano la Bwana kutoka mji wa Daudi, yaani, Sayuni”.*

> *1Nyakati 7:4 “Na pamoja nao, katika vizazi vyao, sawasawa na mbari za baba zao, walikuwapo vikosi vya jeshi la vita, watu thelathini na sita elfu; kwa kuwa wake zao na watoto wao walikuwa wengi”.*

> *1Nyakati 8:28 “Hao ndio waliokuwa wakuu wa mbari za baba zao, katika vizazi vyao vyote, watu maarufu; na hao walikuwa wakikaa Yerusalemu”.*

> *1Nyakati 9:33 “Tena hawa ndio waimbaji, wakuu wa mbari za baba zao katika Walawi, ambao walikaa vyumbani, kisha walikuwa hawana kazi nyingine; kwa kuwa walitumika katika kazi yao mchana na usiku”.*

> *1Nyakati 26:13 “Nao wakatupiwa kura kwa ajili ya kila lango, wadogo sawasawa na wakubwa, kwa kadiri ya mbari za baba zao”.*

> *Luka 1:26 “Mwezi wa sita, malaika Gabrieli alitumwa na Mungu kwenda mpaka mji wa Galilaya, jina lake Nazareti,*
>
> *27 kwa mwanamwali bikira aliyekuwa ameposwa na mtu, jina*

> *lake Yusufu, WA MBARI YA DAUDI; na jina lake bikira huyo ni Mariamu”.*

Soma pia Nehemia 10:34, 11:13

Shalom.

Tafadhali washirikishe na wengine habari hizi njema, na pia kama utapenda tuwe tunakutumia mafundisho ya Neno la Mungu ya mara kwa mara kwa njia ya email yako au Whatsapp basi tutumie ujumbe kwenye namba hii +255693036618 au +255789001312

Mada Nyinginezo:

> *LISHIKILIE SANA LILE AGIZO LA KWANZA.[1]*

> *Nini maana ya “mkilichukia hata vazi lililotiwa uchafu na mwili”?[2]*

Sadaka ya kuinuliwa ni sadaka ya namna gani?[3]

Kwanini Mungu aliwaagiza wana wa Israeli wasikisaze chakula?[4]

Rudi nyumbani:[5]

Share on:
WhatsApp
Endnotes:

1. LISHIKILIE SANA LILE AGIZO LA KWANZA.: https://wingulamashahidi.org/2020/12/23/lishikilie-sana-lile-agizo-la-kwanza/
2. Nini maana ya “mkilichukia hata vazi lililotiwa uchafu na mwili”?: https://wingulamashahidi.org/2020/12/22/nini-maana-ya-mkilichukia-hata-vazi-lililotiwa-uchafu-na-mwili/
3. Sadaka ya kuinuliwa ni sadaka ya namna gani?: https://wingulamashahidi.org/2020/12/20/sadaka-ya-kuinuliwa-ni-sadaka-ya-namna-gani/

4. Kwanini Mungu aliwaagiza wana wa Israeli wasikisaze chakula?: https://wingulamashahidi.org/2020/12/15/kwanini-mungu-aliwaagiza-wana-wa-israeli-wasikisaze-chakula/
5. Rudi nyumbani:: https://wingulamashahidi.org/